EATGN
EAST AFRICAN TAX AND GOVERNANCE NETWORK
MTANDAO WA USHURU NA UTAWALA
WA AFRIKA MASHARIKI

WAJIBU WA MAPATO NA URAIA KATIKA KANDA YA AFRIKA MASHARIKI

Mtazamo wa Haki za Kibinadamu
Zinazohusiana na Ushuru

TAX JUSTICE NETWORK AFRICA

STOP the BLEEDING

Norad

Wajibu wa Mapato na Uraia katika kanda ya Afrika Mashariki

Mtazamo wa Haki za Kibinadamu Zinazohusiana na Ushuru

Imechapishwa na

Kwa Msaada wa

© Mtandao wa Ushuru na Utawala wa Afrika Mashariki (EATGN)

Anwani
Barua pepe: info@eataxgovernance.net / coordinator@eataxgovernance.net
Tovuti: www.eataxgovernance.net

Muundo chapishi

Mwandishi
Okumba Miruka

Chapisho hili linasalia kuwa mali ya EATGN pekee. (2023)

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inayoweza kutolewa, kuhifadhiwa katika mfumo wa kurudufu, au kusambazwa kwa namna yoyote, au kwa njia yoyote ya kielektroniki, kimitambo, kurudufu, kurekodiwa au kwa njia nyinyine yoyote, bila idhini ya moja kwa moja kwa maandishi kutoka kwa mchapishaji. Sehemu yoyote ya chapisho hili inaweza kuhakikiwa au kunukuliwa bila malipo mradi tu asili yake itambuliwe ipasavyo. CHAPISHO HILI SI LA KUUZWA.

KUHUSU EATGN

Mtandao wa Ushuru na Utawala wa Afrika Mashariki (EATGN) unajumuisha Mashirika ya Kiraia, wanaakademia na watu binafsi wenye maslahi anuai katika haki za kifedha ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

EATGN inatambua mahitaji yanaloongezeka ya uelewa wa kina wa ulipaji ushuru ndani ya mijadala ya usimamizi wa fedha za umma, katika kila nchi mwanachama, na kwa ulinganifu wa eneo zima. Hii ni kwa sababu ulipaji ushuru ni muhimili katika ukuaji unaohusiana na maendeleo ya miundombinu, utoaji wa huduma na uzalishaji wa mali.

KUHUSU HAKI ZA BINADAMU NA HAKI YA KODI

Utafiti huu ni mpango unaowezesha kufanyika kwa utafiti wa haki za binadamu katika kuelewa ukosefu wa haki ya kodi katika Afrika Mashariki. Utafiti huu unatarajia kuwavutia wanaakademia, waunda sera, vikundi vya kidini, sekta-binafsi, na Mashirika ya Kiraia, ili kuelewa na kutetea sera bora za kodi ndani ya kigo zao za ushawishi ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

KUHUSU MWANDISHI

Dkt Okumba Miruka ni msomi mwenye digrii ya Elimu (Sanaa), na Uzamili (Sanaa) katika Jinsia na Maendeleo, na Uzamifu (Elimu ya Jinsia na Maendeleo) kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya. Ni msomi wa kimataifa mwenye maarifa na uzoefu katika haki za binadamu, usawa wa jinsia, ufuatiliaji na uhakiki, mipango mikakati, masomo jumuishi, utafiti, na uwekaji wa taarifa. Yeye ni mmoja wa wakufunzi wa haki za binadamu katika Ujenzi wa Kujitegemea katika Haki za Binadamu, kupitia programu ya shirika la Kimataifa la Amnesty, Uholanzi. Dkt Miruka ni mwandishi mwenye machapisho mengi kuhusu jinsia, ukufunzi na fasihi simulizi vinavyosifiwa kwake.

Yaliyomo

1 Utangulizi **7**
1.1 Je, Haki ya Kiuchumi ni nini? 7
1.2 Muhtasari wa Haki za Binadamu 9
1.3 Mbinu inayozingatia Haki za Binadamu (HRBA) 11
1.4 Kanuni za Haki za Binadamu na ulipaji ushuru 12

2 Hatua katika Mkabala wa Haki za Kibinadamu kwa Upangaji wa haki ya kodi **14**
2.1 Hatua ya Kwanza: Uchambuzi wa Sababu
2.2 Hatua ya Pili: Uchambuzi wa haki za walipa kodi na 14
majukumu yao 14
2.3 Hatua ya Tatu: Uchambuzi wa Upungufu wa Uwezo 17
2.4 Hatua ya Nne: Kutambua vipaumbele na kuvitekeleza 17
2.5 Hatua ya Tano: Ubunifu wa Programu 17

3 Mitindo ya Haki za Binadamu katika Ulipaji Ushuru kwa Miktadha ya Dharura **18**

4 Hitimisho **20**

5 Mapendekezo **21**
5.1 Utafiti 21
5.2 Mawasiliano na Usambazaji 21
5.3 Mafunzo na Kujenga Uwezo 21

6 Marejeleo **22**

Orodha ya Majedwali

Jedwali 1: Viungo vya Mfumo wa Ushuru wa Haki 8

Jedwali 2: Je, Ni Nini Lengo la Kazi ya Haki ya Kodi? 13

Jedwali 3: Ulipaji ushuru kama wajibu 17

Shukran
Kuchapishwa kwa utafiti huu kuliwezeshwa na juhudi za Bw Okumba Miruka, mwandishi wa utafiti huu, ambaye kupitia utaalam wake wa kiufundi alifanikisha utafiti huu. Utafiti huu pia haungewezekana bila usaidizi wa kifedha wa Open Society Foundation (OSF) na NORAD chini ya kampeni ya Scaling Up Tax Justice (SCUT) iliosimamiwa na Tax Justice Network Africa (TJNA).

1.0 Utangulizi

Mnamo mwaka wa 2014, Mtandao wa Ushuru na Utawala wa Afrika Mashariki (EATGN) na Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu (KNCHR) walifanya mkutano na serikali za kaunti kuhusu uhusiano kati ya ushuru na haki za binadamu. Majadiliano hayo yalilenga ushuru kama njia ya kuzalisha rasilimali kwa serikali kufikia majukumu ya haki za binadamu katika muktadha wa rasilimali zinazoisha.

Katika kipindi cha mpango-mkakati wa miaka ya 2016 hadi 2018, EATGN ilifanya tafiti kadhaa ikiwa ni pamoja na inayofahamika kama S*era za Haki za Kodi ni Sera za Haki za Kibinadamu*. Chapisho hilo lilitathmini wajibu wa serikali wa kutumia, "rasilimali kamili zinazopatikana" kufikia haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (ESCR). Chapisho hilo lilionyesha jinsi bajeti zilivyotengewa sekta zinazokuza haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni nchini Kenya, Rwanda, Tanzania na Uganda kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

Chapisho hilo lilipendekeza kuwa serikali zinapaswa kuimarisha uwezo wao katika kuzalisha mapato ya ndani kama mkakati wa maana zaidi wa kutekeleza majukumu yao ya haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni. Katika mpango-mkakati wa 2019 hadi 2023, EATGN ilijitolea kuzingatia masuala kadhaa mtambuko ikiwa ni pamoja na vijana, jinsia na haki za binadamu, kwa kupanua shughuli za utafiti, mawasiliano, mitandao, mafunzo na kujenga uwezo. Chapisho hili linajikita katika kujitolea huku kuidadavua dhana ya haki za binadamu kwani inahusiana na ushuru.

Madhumuni ya chapisho hili ni kuonyesha matumizi ya kihatua ya mbinu inayozingatia haki za binadamu (HRBA), kwa haki ya ushuru, ili kuiwezesha EATGN kujumuisha mbinu hiyo katika utenda kazi wake. Pendekezo la dhamana la chapisho hili ni kwamba haki ya ushuru inazingatiwa kuwili.

Kwa upande mmoja, linashughulikia matarajio na mahitaji ya walipa ushuru, hivyo, linafanya haki kwa umma. Kwa upande mwingine, linahitaji kuzingatia mahitaji ya ushuru, ambayo ni haki kwa serikali. Wajibu huu umenakiliwa katika Kifungu cha 29 (5) cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, ambacho kinasema kwamba kila raia binafsi ana wajibu wa *"kufanya kazi kwa kadiri ya uwezo wake wote, na kulipa kodi inayowekwa na sheria kwa maslahi ya jamii".*

EATGN (2017) inasisitiza hili kama ifuatavyo:

> ***...kila raia ana uwezo wa kuhoji serikali yake kwa sababu wanalipa kodi. Hii ni kwa sababu fedha hizi hukabidhiwa kwa mamlaka ili wananchi wapate huduma fulani za msingi.***

Kuelewa haki na wajibu wa kila upande ni jambo la msingi katika kukuza mazingira ambapo usimamizi wa ushuru si mchakato wa kulazimishwa, bali ni shughuli ya pande zote ambapo raia wanatekeleza jukumu lao kama wajibu wa kimaadili, huku serikali zikitumia mapato kwa kujituma, kwa uadilifu na kwa uwajibikaji. Uelewa huu ni muhimu kwa kuelimisha raia juu ya haki na wajibu wao wa ulipaji ushuru na vile vile, kuunda jukwaa la mazungumzo na serikali kuhusu uhusiano wa maana na wenye manufaa ambapo matarajio yanafikiwa na pande zote mbili.

Kuelimisha umma kuhusu haki zao kunapaswa kuchochea kimantiki mahitaji ya haki ya ushuru wakati malipo ya ushuru kwa hiari na kikamilifu yatachangia mapato ya juu kwa serikali, na pengine huduma yawe bora zaidi. Mtindo huu unamweka mwananchi katikati mwa masuala ya ushuru sio tu kama chanzo cha mapato bali pia kama mpigania haki kulingana na maono ya EATGN ya, *"mfumo wa ushuru wa haki, uwazi, uwajibikaji na ulipaji unaoendeshwa na raia"* kama sehemu ya haki ya kiuchumi.

1.1 Kuelewa Haki za Kiuchumi

Haki ya kiuchumi ni mipango inayolenga kuleta mabadiliko ya kimuundo kwa kutoa ndaro kwa dhana kuu za maendeleo na za kidesturi juu ya maendeleo-endelevu. Inalenga kushughulikia vidhihirishi na visababishi

vya ukosefu wa usawa katika mwendelezo wa uzalishaji, ukusanyaji wa mapato, mgao wa bajeti, matumizi ya serikali na usimamizi wa jumla wa rasilimali ili kupunguza pengo kati ya matajiri na maskini. Ajenda ya mabadiliko ya kimuundo ni kuongeza uzalishaji kama hatua ya kwanza katika kuongezeka kwa mapato na ukuaji wa juu wa uchumi.

Katika Afrika Mashariki, mabadiliko ya kimuundo hudhaniwa kuwa uhuru kutoka kwa mifano ya ukoloni ya maendeleo ya kiuchumi kulingana na uchimbuaji unaoelekea katika muundo unaotazamia ndani kwa ndani, na unaoendeleza thamani ya ndani kwa maendeleo ya usawa.[1] Dhana hii imejumuishwa katika kuondoa ukosefu wa usawa wa kodi, unaofafanuliwa kama tofauti ndani ya utaratibu wa ukusanyaji wa ushuru na jinsi unavyoathiri ugawaji na/au matumizi ya fedha za umma na kusababisha usimamizi usiofaa wa mapato ya ndani (DRM).

Kwa mfano, tofauti za kijinsia katika taratibu za ushuru huyatenga makundi fulani kutoka katika fursa za kiuchumi na manufaa na kuzidisha mapungufu.[2] Haki ya kiuchumi inahitaji mfumo wa haki wa ushuru ambao unahusisha, kwa muhtasari viungo vifuatayo.

Haki ya ushuru kwa kifupi, inafafanuliwa kama uhifadhi wa ushuru kwa wale ambao wanastahili, na inaonekana kijuujuu kumaanisha kuwa serikali zina haki ya kutoza na kukusanya ushuru.[3] Katika ngazi ya pili, hata hivyo, ina maana kwamba walipa ushuru wanaweza na wanapaswa kudai huduma kutoka kwa

Viungo vya Mfumo wa Haki wa Ushuru[4]

1. **Kila mtu analipa kiasi cha ushuru kulingana na uwezo wake -** Kadiri unavyopata mapato mengi na unavyomiliki (mali) zaidi, ndivyo unapaswa kulipa zaidi. Viwango vya juu vya ushuru vinavyotumika kwa kila mtu (kama vile ushuru wa matumizi) huwaumiza maskini zaidi. Kwa viwango sawia, ushuru zaidi unapaswa kukusanywa kutoka kwa watu na makampuni moja kwa moja kuliko kutoka kwa kila mtu kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

2. **Hakuna uvujaji wa mapato -** Mapato mengi yanayoweza kukusanywa hupotea kwa sababu ya kutoa vichocheo vya ushuru na mikataba isiyo ya lazima ambayo hainufaishi nchi ambako faida hutolewa. Kukomesha vichocheo vya ushuru visivyo vya lazima na kuhakikisha kwamba mikataba ya ushuru inaruhusu kubakizwa kwa haki zetu nyingi za utozaji ushuru, na kuhakikisha kwamba tuna mapato zaidi.

3. **Ushuru unatumiwa kustawisha maisha ya watu -** Mapato ya kodi yanapaswa kutumiwa katika kuimarisha sekta za kijamii kama vile afya, elimu, na ulinzi wa mazingira katika maeneo haya ambayo yanakuza usawa. Watu wanapolipia afya na elimu yao, wanabaki na pesa kidogo za kukidhi mahitaji yao, kuweka akiba na kuwekeza.

4. **Uwazi, uwajibikaji, sawa, na rahisi -** Watu wanapaswa kujua ni kiasi gani cha ushuru wanapaswa kulipa na jinsi gani. Iwapo hawatajua, itakuwa vigumu kutii. Pia wanahitaji kushiriki katika jinsi kodi zinavyotekelezwa na kutumika. Dhana ya 'fedha za serikali' ni potofu. Kuna 'fedha za walipa kodi' pekee, hivyo, kuna hitaji la ushiriki wa wananchi katika masuala ya kodi.

1. Onyango CH, *Promoting Equity Through Structural Transformation: Impact of Free Trade Agreements on East African Regional integration*, Econews Africa: 2020 https://econews-africa.org/wp-content/uploads/2020/06/Final-Trade-Summary-Report-2-1.pdf
2. EATGN, *Intersectionality, Marginalisation and Gender Tax Inequality in Kenya : A Working Paper*, 2019, https://www.eataxgovernance.net/wp-content/uploads/2020/03/r2-Intersectionality-Marginalisation-and-Gender-Tax-Inequality-in-Kenya-003-1.pdf.
3. Juhudi au mipango ya jumla ya kushughulikia madhihirisho mbalimbali ya ukosefu wa usawa ndani ya taratibu za ukusanyaji, ugawaji, matumizi, na usimamizi wa kodi ili kuziba pengo kati ya matajiri na maskini pamoja na kufikia uhamasishaji wa mapato ya ndani kwa ajili ya kujitosheleza.
4. Katindi SN, Thinking for the Future East Africa Tax Strategic Planning Workshop Report, Nairobi: EATGN, 2019, https://www.eataxgovernance.net/wp-content/uploads/2020/03/R-Thinking-for-the-Future-East-Africa-Tax-Strategic-Planning-Workshop-Report.pdf

serikali ambayo ipo mamlakani kusimamia mambo ya serikali kwa niaba ya raia. Hii inajumuisha uhusiano ambao serikali na raia wote wana haki fulani (pia huitwa madai) na wajibu (pia huitwa kazi).

Hili likoje? Serikali ina madai halali kwa raia kulipa kodi kwa bidii na uaminifu kama inavyofafanuliwa katika sheria au hatua za kifedha. Katika muktadha huu, raia wana majukumu wanayobeba. Lakini serikali pia ina wajibu wa kutoa bidhaa na huduma kama vile usalama, afya, masomo, miundombinu na maji. Katika muktadha huu, wananchi ndio wenye madai au haki. Hivyo basi, majukumu ya watekelezaji wajibu na wenye madai au haki hayabaki palepale bali yanabadilika kulingana na muktadha.

Haki na wajibu vinaweza kubainishwa zaidi na masuala ya jinsia kwa kuwa mambo fulani huathiri wanawake tofauti na wanaume. Kwa mfano, hedhi huathiri wasichana na wanawake pekee. Kwa hivyo, kutozwa ushuru kwa sondo kunaathiri kufurahia kikamilifu haki za usafi wa hedhi. Wanawake na wasichana, kwa hivyo, wana dai kwa serikali kutoa sondo bure, kuondoa ushuru wazo au kuomba ruzuku ili kufanya bidhaa hizo kununulika.

1.2 Muhtasari wa Haki za Binadamu

Juhudi za kufafanua haki za binadamu nizaweza kurejewa kwa mwanasheria wa Marekani Wesley Newcomb Hohfeld, ambaye ndiye aliyekuwa wa kwanza kujaribu kuondoa ugiligili kuhusu jinsi wasomi wa sheria walivyolifafanua neno 'haki'. Alidai kwamba *"haki zinarejelea haki za kudai, kwa kuwa zinajumuisha wajibu*

Je, Ni Nini Lengo la Kazi ya Haki ya Kodi?

1. **Kubadilisha Kanuni -** Kupitia uanachama wa Mtandao wa Haki ya Ushuru Afrika (TJNA), EATGN iko mstari wa mbele katika kupiga vita ukosefu wa usawa katika masuala mbalimbali yanayodhihirisha tofauti zinazohusiana na tija ya kazi na ufanisi wa mgao wa uchumi kwa kuzingatia jinsi ushuru inavyoathiri malipo kwa kazi; rasilimali watu; upatikanaji wa mtaji; na udhibiti wa rasilimali nyingine za uzalishaji.

2. **Kuhusisha Sheria -** EATGN inasaidia mtandao wa TJNA kupitia uratibu wa shughuli za utetezi zinazohusu madai ya maslahi ya umma (PIL). TJNA iliwasilisha ombi kwa Mahakama Kuu ya Kenya ambalo lilifanikisha kupatikana kwa Makubaliano ya kuepuka kulipa ushuru maradufu (DTAA) kati ya Kenya na Mauritius, kuwa kinyume cha Katiba. Huu ni uamuzi muhimu barani Afrika unaohitaji makubaliano ya DTAA kuwa chini ya michakato ya uidhinishaji inayohitajika kikatiba. Uamuzi huu unatumika kama hatua ya kwanza katika kuhakikisha mashauriano yanayofaa na mapana ya washikadau kuhusu masuala yenye maslahi kwa taifa.

3. **Uzalishaji wa Maarifa -** EATGN imechapisha tafiti kama vile *"Intersectionality, Marginalisation and Gender Tax Inequality in Kenya - A Working Paper"; "Nairobi International Financial Centre, or Nairobi Tax Haven?"* na *"THE NEXUS BETWEEN INTERNATIONAL TRADE AND TAX GOVERNANCE: An Assessment of Tax Regulations in The East African Community".* Wakati huo huo, TJNA imechapisha tafiti kama vile *"TRICK OR TREAT(Y)?" "Kenya's Tax Treaty Giveaways to Tax Heavens,"* miongoni mwa zingine. Utafiti huo unalinganisha masharti katika Falme za Kiarabu, Uholanzi na Mauritius, Makubaliano kuhusu Kodi Maradufu (DTA) na Kenya kuhusiana na vifungu vya DTA vya mifano muhimu ya kodi kama vile Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), Umoja wa Mataifa (UM) na Jukwaa la Usimamizi wa Ushuru Afrika (ATAF).

4. **Ubia -** EATGN inataka kujenga msingi wa wanachama mbalimbali kwa kutambua kwamba kufikia mabadiliko katika ngazi ya Afrika Mashariki, mkakati wa kujenga muungano, na maendeleo ya ushirikiano ni muhimu. Kuingia ubia na mashirika yenye nia moja katika eneo hili na duniani kote kutawezesha uanachama wake kukua na kuupa mtandao washirika thabiti ili kuendeleza malengo ya haki ya ushuru.

wa uwiano wa watu au vikundi kutenda au kuacha kutenda kwa njia zinazohitajika kwa wenye haki" (Hohfeld, 1913, 1917). *Haya yalisemwa tena na Joel Feinberg ambaye alitanabai kwamba "kuwa na haki ni kuwa na madai dhidi ya mtu, ambayo kutambuliwa kwake kama halali, kunahitajika kuzingatia jozi fulani ya sheria au kanuni za maadili"* (Feinberg, 1970). Fasili hizi zina maelezo sawa ya; *madai na wajibu*.

Amnesty International (2010) inafafanua haki za binadamu kama, *"viwango vya msingi ambavyo bila kuwa navyo, watu hawawezi kuishi maisha ya hadhi kama binadamu"*. Muhimu katika ufafanuzi huu ni dhana mbili. Ya kwanza ni "viwango" ambayo inarejelea kaida za msingi. Ya pili ni "hadhi" ambayo inahusu thamani. Kwa hivyo, haki za binadamu huainisha masharti fulani yasiyopungua, ambayo, kwa upungufu wake maisha hayatakubalika na hayatawiana na thamani ya binadamu.

Kama ilivyoelezwa na Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa (UM), Koffi Annan, lengo kuu la haki za binadamu ni kuhakikisha uhuru kutoka kwa woga na uhitaji. Kwa kifupi, haki za binadamu hufafanua jinsi tunavyopaswa kuwatendea na kutendewa na wengine, na kile tunachopaswa kutarajia katika mwingiliano wetu na kuishi pamoja.

Kwa madhumuni ya utambulisho na uainishaji, haki za binadamu kwa kawaida zimepangwa katika makundi matatu:

1. **Haki za kiraia na kisiasa (CPR)** zinarejelea haki zinazohusiana na maisha yetu, watu binafsi na uhuru ambao ni lazima utimizwe mara moja. Zinaweza pia kuitwa mambo ya msingi ambayo hayapaswi kuingiliwa. Kwa maana hii, zinajulikana pia kama "haki hasi" kwa sababu zinazuia serikali na vyombo vingine kuingilia kati kufurahia haki hizi. *Haki za Kiraia na Kisiasa(CPR)* ni pamoja na haki ya kuishi, uhuru, usalama, utaifa, na kushiriki katika uchaguzi kama mpiga kura na/au mgombea. Zinajumuisha pia uhuru kutoka kwa utumwa, kazi ya kulazimishwa na uhuru wa mawazo, dhamiri, dini, uwanaharakati, na ushirika wenye amani. Pia zinajumuisha usawa mbele ya sheria. Azimio la Mapinduzi ya Ufaransa la Haki za Binadamu na Haki za Raia (1789) lilitoa muhtasari wa haki hizo kuwa uhuru, usawa, na udugu-jumui. Haki za Kiraia na Kisiasa zinajulikana pia kama "haki za kizazi cha kwanza", na zimejumlishwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (1966).
2. **Haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni** (ESCR) zinarejelea haki zinazohusiana na vitu vya hali ya maisha kama vile; chakula, afya, makazi, elimu na usalama wa kijamii. Haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni kwa kawaida, zinazojulikana kama haki za maendeleo, na ni za mwelekeo chanya kwa sababu zinahitaji serikali iingilie ili ziweze kutimia kwa njia ya maana. Haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni pia hujulikana kama "haki za kizazi cha pili" na zimejumuishwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (1966).
3. **Haki za kindugu** zinarejelea haki za pamoja. Zinajumuisha haki za rasilimali zinazotumiwa kwa pamoja kama vile mazingira safi na yenye afya ya kibayolojia na angahewa, kujiamulia, urithi wa kitamaduni, na maendeleo endelevu. Wazo hilo lilienezwa na mwanasheria wa KiCzech Karel Vasak, katika Taasisi ya Kimataifa ya Haki za Kibinadamu,1979 huko Strasbourg. Haki hizi zimetawanywa katika vyombo vya haki za binadamu vya kikanda na vya kimataifa iwe vinahusika na Haki za Kiraia na Kisiasa (CPR), au na haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (ESCR). Pia mara nyingi hujulikana kama "haki za mshikamano" au "haki za kizazi cha tatu".

Uainishaji na uwekaji kumbukumbu wa haki za binadamu hapo juu unazipa umbo na kufafanua uhusiano kati ya wahusika wanaoweza kuzidai (wenye haki) na wale wanaopaswa kuhakikisha kuwa zinafurahiwa kikamilifu (wenye wajibu). Mwenye wajibu mkuu ni serikali kwa kuwa ndiyo chombo kinachoidhinisha sheria za haki za binadamu. Katika hali halisi, hata hivyo, yeyote anayehusika na kuhakikisha haki inatendeka ndiye mwenye wajibu.

Mataifa yana majukumu matatu ya kimsingi kuhusu haki za binadamu ambayo ni; *Kuheshimu, Kulinda* na *Kutimiza* kama ifuatavyo:

1. Wajibu wa *kuheshimu* unaihitaji serikali kutoingilia utekelezwaji wa haki. Kwa mfano, Serikali inapaswa kuwaacha raia wachague dini watakayoifuata.
2. Wajibu wa *kulinda* unaipa serikali jukumu la kuzuia watu wengine kuingilia kati utekelezwaji wa haki. Kwa mfano, ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa mwanachama wa chama cha siasa cha wachache hanyanyaswi na wafuasi wa chama wa walio wengi.
3. Wajibu wa *kutimiza* unaweza kugawanywa katika majukumu mawili mahususi zaidi; yaani *kuwezesha* na kutoa.
   a) Wajibu wa *kuwezesha* unahitaji serikali kuunda hali zinazowawezesha wenye haki kutambua haki zao. Kwa mfano, kwa kuwapea mafunzo, kuwaajiri, na kuwalipa walimu, serikali inawawezesha watoto kutambua haki yao ya kupata elimu.
   b) Wajibu wa *kutoa* unaipa serikali jukumu la kusambaza bidhaa au huduma moja kwa moja kwa wale ambao hawawezi kuzalisha, kumudu, au kuzipata na ambao ubinadamu wao unatatizika. Kwa mfano, chakula cha msaada huhakikisha kwamba haki za watu walio katika dhiki zinazingatiwa. Vile vile, kuwatumia fedha wazee na watoto walio katika mazingira magumu kunahakikisha kwamba wanaweza kukidhi mahitaji yao ya msingi na kuishi maisha ya hadhi.

Haki za binadamu zinafafanuliwa zaidi kuwa zina sifa nne.
1. Kwanza ni kwamba *ni za kuzaliwa*. Hii ina maana kwamba ni za asili na zinatumika kwa wanadamu wote na hazipatikani kutoka nje wala kupeanwa na mtu.
2. Pili ni kwamba ni za *Kilimwengu*. Hii ina maana kwamba haki za binadamu ni za kila mtu kila mahali bila kujali asili, rangi, kabila, jinsia, umri, dini, imani, maoni ya kisiasa, hali ya kiuchumi, au ubainisho mwingineo.
3. Tatu ni kwamba haki za binadamu *haziwezi kubatilishwa*. Haziwezi kuondolewa kwa vile hazijatolewa na mtu yeyote. Hata hivyo, haki fulani zinaweza kuwekewa mipaka kisheria na Serikali.
4. Mwisho ni kwamba haki za binadamu *hazigawanyiki* na *zinategemeana*. Hii ina maana kwamba ingawa zimeainishwa na kuratibiwa kwa njia tofauti, haki za binadamu zinahusiana na hazitenganishwi, hivyo basi, kutekelezwa kwa moja kuna uhusiano usioweza kutenganishwa na nyingine.

Kwa njia nyingine, ukiukaji wa haki moja bila shaka huhatarisha haki nyingine. Kwa mfano, ukiukaji wa haki ya chakula kunahatarisha haki za afya na maisha.

1.3 Mbinu inayozingatia Haki za Binadamu (HRBA)

Mabadiliko katika mbinu zinazozingatia haki za binadamu yanahusiana na mijadala juu ya jinsi maendeleo yanapaswa kudhaniwa. Kwa upande mwingine ni nadharia kwamba maendeleo ni *njia ya kukabiliana na upungufu uliomo katika hali ya binadamu*. Hii inajulikana kama mbinu inayozingatia mahitaji. Mahitaji haya ni ya kimsingi na yanaweza kutimizwa kupitia uandalizi wa moja kwa moja kama vile chakula na malazi. Wakala uko kwenye uandalizi. Kwa upande mwingine, mbinu hii inayozingatia haki, ambayo *hutoa matakwa ya hali ya binadamu*. Wakala hapa upo kwenye mmiliki wa haki.

Mahitaji ya watu hayafanani, ila yanatofautiana kulingana na mahali, muktadha, na hali ya mtu binafsi. Kwa mfano, baadhi ya wananchi wanapokuwa na njaa katika sehemu moja ya nchi kwa kukosa chakula, wengine katika sehemu nyingine ya nchi wanapata chakula kwa wingi. Kwa hivyo, usambazaji wa msaada wa chakula utaelekezwa tu kwa walio na njaa. Lakini haki za kibinadamu ni za kimataifa. Kwa mfano, hata kama hali ya maisha inaweza kutofautiana, kila mwanadamu anahitaji kiwango fulani cha chini kabisa cha chakula ili kuishi. Mahitaji hutimizwa huku haki zikiafikiwa. Hii ina maana kwamba ingawa mahitaji yanahusiana na maisha halisi , haki zinahusiana na hali za kudhaniwa za kibinadamu.

Chakula kama mahitaji, ina maana kinapatikana ili kudumisha uhai. Lakini chakula kama haki ina maana kwamba kiwe cha kiwango na ubora fulani kuhakikisha maisha yenye afya. Hivyo, mahitaji kwa kiasi kikubwa ni ya kiwango ili hali haki zinazingatia ubora. Vile vile, mahitaji hayahitajiki kuhusisha wajibu

lakini haki inahusisha. Kwa mfano, kuwa na njaa (kuhitaji chakula) haimaanishi serikali ina jukumu la kukupa mahitaji yako. Lakini wakati uwezo wako wa kujipatia chakula unatoweka kwa kiasi kwamba njaa inahatarisha maisha yako, basi serikali ina wajibu wa kuingilia. Kukosa kufanya hivyo ni ukiukaji wa haki zako. Kwa hivyo, mbinu inayozingatia haki za binadamu inaegemea kanuni kwamba utoaji wa bidhaa na huduma kutoka kwa serikali si tendo la ukarimu bali ni wajibu. Dhana za waliokabiliwa mamlaka na utekelezaji wa haki humaanisha wana mkataba wa kijamii wenye matarajio na wajibu. Kwa hivyo Mbinu inayozingatia Haki za Binadamu (HRBA) ni mchakato wa kimfumo wa kuainisha uhusiano kati ya madai halali ya wenye haki na wajibu wa watekelezaji.

Kupitishwa kwa Mbinu inayozingatia Haki za Binadamu kulichapuzwa baada ya mwaka wa 1997 wakati Koffi Annan alipozindua programu ya mabadiliko katika Umoja wa Mataifa na, miaka miwili baadaye, akatangaza kwamba *"kukuza na kulinda haki za binadamu kupo katika kiini cha kila sehemu ya kazi yetu na kila kipengele cha Mkataba wetu"*. Kauli hii ilitafsiriwa kuwa kanuni za programu kwenye mkutano wa Umoja wa Mataifa mwezi Mei 2003 ambao ulikubalina kwamba mipango yote ya ushirikiano wa maendeleo, sera na usaidizi wa kiufundi inapaswa kuendeleza uafikiaji wa haki za binadamu, kwa kuongozwa na kanuni zilizoorodheshwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu na vyombo vingine vya kimataifa kuhusu haki zabinadamu.

Kwa hivyo, kuchangia katika kukuza uwezo wa 'wanaotekeleza wajibu' kutimiza wajibu wao na wa 'wenye kumiliki haki' kudai haki zao. Kutokana na hili, mkutano wa Umoja wa Mataifa uliorodhesha zifuatazo kama sifa za msingi za mbinu, ambazo zinafahamisha mbinu inayozingatia haki za binadamu kam ilivyoelezwa katika sehemu za baadaye za chapisho hili:

a) Tathmini na uchambuzi wa madai, majukumu yanayoandamana na mfuatano wa sababu zinazoathiri hali ya mwanadamu.
b) Tathmini ya uwezo wa wenye haki kudai haki zao, na kazi ya wamiliki wa ofisi kutimiza wajibu wao ikifuatiwa na mikakati ya kuzijenga.
c) Ufuatiliaji na tathmini ya michakato na matokeo ya vitendo vinavyoongozwa na viwango na kanuni za haki za binadamu.
d) Umisingi ya programu zilizopendekezwa na mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu pamoja na mbinu.

1.4 Kanuni za Haki za Binadamu na ulipaji ushuru

Mbinu inayozingatia Haki za Binadamu inasisitiza kwamba si lazima maendeleo yazingatie tu matokeo bali pia uhalali wa michakato inayotumika kuyatimiza. Matokeo ya kupendeza kwa kiasi kidogo yanarejelewa kuwa *viwango vya haki za binadamu* (kwa mfano, kila binadamu ana haki ya kiwango fulani cha chini cha chakula na virutubisho kwa siku). Michakato halali inaitwa *kanuni za haki za binadamu* (kwa mfano, wale wanaotoa msaada wa chakula hawapaswi kubagua yeyote aliye na uhitaji). Viwango hivyo vimebainishwa katika sheria za kimataifa za haki za binadamu huku kanuni zikiwekwa kwa njia tofauti lakini zinalingana na vipengele vitano vilivyo vilivyofupishwa hapa chini na kiambatisho–KITITA: (Ushiriki, Uwajibikaji, Kutokubagua, Uwezeshaji, na utawala wa Sheria).

a) Ushiriki unahitaji kuwajumuisha wenye haki katika kueleza mawazo yao na kushawishi michakato ya kufanya uamuzi. mawazo na kushawishi michakato ya kufanya maamuzi.
    - Kama ilivyonakiliwa na Bagenda (2011), *"msimbo wa ushuru ambao umefikiriwa na kuundwa kwa namna ambayo inahusisha waunda sera pekee huku ukiyatenga makundi ya jamii za kiraia na umma mpana...hauwezi kusemwa kuwa unaambatana na Mbinu Inayozingatia Haki za Binadamu"*.

b) Uwajibikaji unarejelea umuhimu kwa wanaotekeleza majukumu kutumia rasilimali kwa uadilifu, kutoa ripoti na kuchunguzwa au kuwekewa vikwazo. Raia wana haki ya kudai hivyo.
c) Kutokuwa na mapendeleo kunamaanisha kwamba wanaotekeleza majukumu hawaegemei upande wowote katika utoaji wa huduma.

d) Uwezeshaji unahitaji kwamba wenye haki wasidhalilishwe bali waelimishwe na uwezo wao ujengeke ili kuwajibisha mamlaka.
e) Utawala wa Sheria unamaanisha kwamba hakuna mapuuza ya sheria, ufisadi, au kukwepa mshakato wa kisheria.

Ikiwa mojawapo ya kanuni zilizo hapo juu hazitazingatiwa, mchakato mzima una kasoro. Jedwali hapa chini linaonyesha matumizi ya kila kanuni katika ulipaji ushuru na athari kwa serikali na walipa ushuru.

Jedwali la 3: Utumiaji wa Kanuni za Ushuru: Athari kwa Serikali na walipa kodi

Kanuni za mbinu zinazozingatia haki za Binadamu	Athari kwa Serikali	Athari kwa mlipa kodi
1. Kushiriki	• Ruhusu wananchi kueleza vipaumbele vyao kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya mwaka. • Wasilisha mapendekezo ya hatua za ushuru kwa mjadala wa umma	• Hudhuria vikao vya majadiliano ya bajeti. • Wasilisha vipaumbele vya bajeti. • Chunguza bajeti ili kujumuisha vipaumbele vilivyopendekezwa na uwezekano kuwa mzigo kwa walipaushuru
2. Kuwajibika	• Eleza jinsi ambavyo mapato yamegawanywa na kutumika • Washtaki maafisa wa serikali ambao ni wafisa	• Hakiki hesabu za serikali • Dai maelezo juu ya miradi ambayo haijakamilika • Toa taarifa za visa vya ufisadi • Dai mashtaka kwa viongozi fisadi wa serikali
3. Kutobagua	• Toza ushuru bila mapendeleo • Funga njia za kukwepa kulipa ushuru • Gawa rasilimali za umma kwa usawa katika maeneo yote.	• Dai kutopendelewa na mamlaka ya ushuru. • Hoji ugavi wenye mapendeleo wa rasilimali na miradi ya maendeleo
4. Uwezeshaji	• Elimisha walipa ushuru kuhusu haki na majukumu yao • Toa mafunzo kwa walipa ushuru juu ya kukokotoa ushuru na kuwasilisha mrejesho wa ushuru wao • Orodhesha mawakala wa ushuru walio na leseni • Elimisha wananchi kuhusu taratibu za kutatua migogoro ya ulipaji ushuru. • Chapisha sheria za ushuru	• Kuelewa sheria za ushuru • Kudhuria mabaraza ya kuelimisha walipa ushuru. • Kutumia njia za kutatua migogoro ya ushuru. • Kutoa mrejesho kwa mamlaka ya ushuru
5. Kufuata sheria	• Toza ushuru makato ya kisheria pekee • Jiepushe na unyanyasaji wa kholela kwa walipa ushuru • Heshimu maamuzi ya mahakama kuhusu migogoro ya ushuru.	• Pinga utozaji ushuru usio halali na usiofaa kupitia mahakama za sheria. • Tii maamuzi ya mahakama kuhusu mizozo ya ushuru au kata rufaa.

2.0 Hatua katika Mkabala wa Haki za Kibinadamu kwa Upangaji wa haki ya Ushuru[5]

Kuna hatua kadhaa za kimantiki zinazofuatwa katika kutumia Mbinu Inayozingatia Haki za Binadamu. Kila moja imeelezwa hapa chini na mifano kulingana na kulipa ushuru.

2.1 Hatua ya Kwanza: Uchambuzi wa Sababu

Huu ni mchakato ambapo tatizo huchambuliwa kwa kutambua mwandamo wake kutoka kwa iliyo kuu zaidi, yenye madhara kiasi na hatimaye isiyo mbaya sana. Hii inalenga kutenga sababu kuu au chanzo kikuu kinachohitajika kuondolewa badala ya kushughulikia dalili. Kwa mfano, dalili inaweza kuwa mamlaka ya ushuru mara kwa mara inashindwa kufikia malengo yake ya kukusanya mapato yanayohitajika. Hii ina maana kwamba serikali haipati rasilimali za kutosha kufadhili programu zake za maendeleo.

Ni zipi sababu kuu zaidi za hili? Moja inaweza kuwa walipa ushuru tarajiwa wanaweza kuwa hawajasajiliwa (kwa mfumo wa kulipa ushuru) kwa hivyo, hawalipi sehemu yao ya ushuru. Hii inaweza kuhusishwa na mtazamo usiofaa kuhusu ulipaji ushuru kutokana na imani kwamba ni njia ya kuwadhulumu raia kwa kuwanyang'anya mapato yao, serikali kukosa kutoa huduma na uzoefu wa ubaguzi katika usambazaji wa miradi ya maendeleo.

Uchambuzi huu unatuelekeza katika vianzo vya msingi wa shinda kama: uhusiano hasi kati ya mamlaka ya ushuru baina ya walipa ushuru; rushwa ili kukwepa kulipa ushuru; kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa kisheria; na uingiliaji wa kisiasa katika usimamizi wa ushuru na ugawaji wa rasilimali. Kila kimoja cha vianzo hivi kinaweza kushughulikiwa kupitia mikakati ya muda mfupi. Lakini suluhisho la kudumu ni kutatua sababu zilizokita zaidi.

2.2 Hatua ya Pili: Uchambuzi - Ruwaza

Uchambuzi ruwaza unahusu kutenganisha uhusiano baina ya wenye madai na wenye wajibu kwa kuzingatia haki na majukumu yao. Hili linabainisha uhusiano wa moja kwa moja kuhusu matatizo na chanzo chake. Kwa mfano, serikali kutopata kodi ya kutosha, kunahitaji upanuzi wa wigo wa utozaji ushuru. Hii ina maana kwamba mamlaka ya ushuru ina madai halali kwa biashara ambazo hazijajisajili na kuanza kulipa ushuru. Kwa hivyo biashara kama hizi zina wajibu wa kujisajili ili kuweza kulipa kodi zao ipasavyo. Lakini pia wana haki ya kudai mamlaka ya ushuru, kuweka utaratibu wa usajili ifaavyo. Katika utaratibu huu, madai ya mlipa ushuru ni sawa na wajibu wa mbeba jukumu.

Uhusiano wa haki na wajibu kati ya mamlaka ya ushuru na walipa ushuru umebainishwa katika mikataba ya huduma ya mamlaka mbalimbali za mapato katika Afrika Mashariki. Uchambuzi wa mikataba ya Kenya, Uganda na Rwanda unaonyesha serikali hizo zinatambua haki za walipa ushuru kupata taarifa; kuweka siri na uaminifu, kuwakilishwa na wakala wa ushuru na/au wakili wa kisheria; maamuzi ya migogoro yaliyotolewa na mamlaka ya ushuru; kudhaniwa kuwa na uaminifu; na kutendewa kwa heshima na adabu na maafisa wa ushuru.[6] Mkataba wa Tanzania inatambua haki hizi zote lakini upo kimya kuhusu haki za kuwakilishwa na kutendewa kwa heshima na adabu. Ufuatao ni ufafanuzi wa haki na majukumu yanayohusiana na mamlaka ya mapato.

- ***Haki ya Kupata Taarifa:*** Walipa ushuru wana haki ya kupata taarifa sahihi kuhusu haki zao za ulipaji ushuru, wajibu na taratibu za kufuata katika kuzitimiza. Hili linahusisha haki ya kuelimishwa na mamlaka ya mapato, kupata maelezo kuhusu usimamizi wa kodi, kupata sababu za maamuzi yaliyofanywa, kupokea ujumbe mapema kwa ajili ya ukaguzi wa kawaida na ukaguzi wa jumla na kupata majibu kuhusu maswali na malalamiko yaliyowasilishwa. Pia wana haki ya kujua kiasi cha ushuru kinacholipwa kwa kila sehemu ya mapato. Wajibu unaohusiana wa mamlaka ya mapato ni kufanya taarifa kuwapo na

5. Utaratibu huo umefafanuliwa katika Jonsson, 2003. Ona pia Christian Aid & SOMO, Tax Justice Advocacy: A Toolkit for Civil Society, 2011, https://www.christianaid.org.uk/sites/default/files/2022-09/tax-justice-advocacy-toolkit-jan-2011.pdf
6. Taarifa kutoka Burundi na Sudan Kusini hazikupatikana.

ipatikane kupitia mifumo mbalimbali. Pia ina jukumu la kuweka akaunti sahihi za walipa ushuru wote na kuifanya ipatikane kwao.

- ***Haki ya siri na uaminifu:*** Mamlaka ya ushuru hukusanya na kuweka maelezo ya kina kuhusu walipa ushuru. Hawa wana haki ya taarifa hizi kuwekwa salama na sizifichuliwe kwa wahusika wasioruhusiwa. Wajibu unaohusiana wa mamlaka ya ushuru ni kuanzisha mifumo ya kulinda taarifa za walipa ushuru na kutoa mafunzo na kuwafungamanisha wafanyakazi wake kudumisha usiri huu. Utunzaji mbaya wa taarifa hizi unaweza kuharibu sifa za walipa ushuru na mamlaka ya mapato, hivyo, kusababisha mashtaka yenye gharama kubwa za kisheria.
- ***Haki ya kuwakilishwa:*** Raia wa kawaida si mtaalamu wa utozaji ushuru na huenda asijue wajibu wake kamili, haki na mbinu za kutatua mizozo ya ushuru , au hata jinsi ya kukokotoa madai ya ushuru , kutoa taarifa ya mapato na kodi au kudai kurejeshewa pesa. Katika hali hii, walipa ushuru wana haki ya kupata huduma za mawakala wa ushuru na wataalam wa kisheria. Wajibu unaohusu mamlaka ya kodi ni kuunda rejista ya mawakala walioidhinishwa/mawakala wenye leseni, kuanzisha njia za mawasiliano nao na kutoa maelezo ya kutosha kuhusu hatua za ulipaji ushuru, sera na kanuni.
- ***Haki ya Kufuata Sheria:*** Mizozo huzuka kati ya walipa kodi na wasimamizi wa ushuru kuhusu masuala kama vile kuripoti kodi, kutolipa kodi, malipo yaliyochelewa, kutozwa ushuru kupita kiasi na ukaguzi wa akaunti za walipaushuru . Walipa ushuru wana haki ya kupinga uamuzi unaotolewa na mamlaka ya mapato, kuwasilisha malalamishi na kuhitaji kusikilizwa ili kupata suluhisho linalofaa. Hili lisipotoa suluhu, wana haki ya kuyaendea mabaraza ya rufaa za kodi na mahakama za sheria. Wajibu unaohusiana wa mamlaka ya ushuru ni kuwapa walipa ushuru nafasi ya kufuata njia hizi na kuacha kuchukua hatua yoyote mbaya dhidi yao kabla ya suala hilo kutatuliwa.
- ***Haki ya Kudhaniwa kuwa Mwaminifu:*** Mamlaka ya ushuru inategemea walipa ushuru kutangaza mapato, kukokotoa madeni yao, kulipa ushuru unaodaiwa na kutoa ripoti ya mapato na kiwango cha ushuru. Walipa ushuru wanadhaniwa kuwa waaminifu katika kufanya hivi isipokuwa kama mamlaka ya ushuru ina ushahidi kuhusu udanganyifu. Ni haki ya walipa ushuru kutazamwa kwa dhana hiyo. Wajibu wa mamlaka ya ushuru ni kutoa sababu za kutilia shaka ushuru uliotangazwa na kuitisha majadiliano ili kutatua mzozo.
- ***Haki ya Kutopendelewa usawa na kwa Haki:*** Mlipa ushuru ana haki ya kutobaguliwa na mamlaka ya mapato na kutendewa kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, mamlaka ya mapato ina wajibu wa kueleza sheria ya ulipaji ushuru kwa usahihi, kuitumia kila mara kwa walipa ushuru wote na kuunda viwango vya kisheria vya usimamizi wa ushuru. Hii ni pamoja na kudai tu kiasi kinachofaa cha kodi na kufanya hivyo kwa njia ambayo si ya kumdhuru mlipa kodi.
- ***Haki ya Heshima na Staha:*** Mlipa kodi ana haki ya kupewa heshima na maafisa wa ushuru na kuhudumiwa kwa staha. Wajibu wa mamlaka ya mapato ni kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake kuhusu kuwahudumia wa walipa ushuru kitaalamu.

Hati za huduma za mamlaka ya mapato ya Afrika Mashariki pia zinaorodhesha wajibu ufuatao wa walipa ushuru:

- ***Usajili:*** Walipa kodi wana wajibu wa kujisajili kwa hiari na mamlaka ya mapato ambapo hii inajumuisha utoaji wa jina, namba ya kitambulisho, anwani na aina ya shughuli za kiuchumi. Wajibu unaohusiana wa mamlaka ya ushuru ni kumpa mlipa ushuru cheti cha usajili. Nchini Rwanda, mlipa ushuru anatakiwa kutekeleza usajili huo ndani ya siku saba baada ya kuanza biashara na kuwa na nambari moja ya kitambulisho cha ushuru.
- ***Kutoa ripoti ya mapato na kodi ya kulipa:*** Walipa ushuru wana wajibu wa kulipa ushuru sahihi na kwa muda uliowekwa, na kuwasilisha nyaraka kwa mamlaka ya ushuru kwa ajili ya rekodi. Dai la mamlaka ya kodi ni kwamba walipa ushuru hutii tarehe na miundo iliyowekwa ya malipo ya ushuru na kutoa ripoti za mapato na kiwango cha ushuru.
- ***Usahihi na Ufichuzi:*** Mlipa ushuru ana wajibu wa kutangaza mapato yote kwa ajili ya kukokotoa kodi na kutoa madai sahihi ya kurejeshewa pesa. Dai la mamlaka ya ushuru ni kwamba mlipa ushuru hutoa taarifa kamili na kwa uaminifu kulingana na mapato yote, na kutoa hati za kuunga mkono ripoti yake ikiwa kuna shaka.

Majukumu mengine yaliyotajwa katika baadhi ya mikataba ya huduma ni ushirikiano na kuwatendea kwa staha maafisa waushuu ; taarifa za ukwepaji kulipa ushuru na makosa mengine; taarifa za bidhaa zinazomilikiwa wakati wa kuwasili kwenye viwanja vya kuingilia nchini; madai ya risiti za kifedha; kuhifadhi na kutoa taarifa za bakaa la ushuru kwa wale wanaostahili kufanya hivyo.

Wajibu wa mamlaka ya mapato unaoladana na haya ni kuanzisha mifumo na vifaa vya kuwawezesha walipa ushuru kutekeleza yaliyo hapo juu. Haya yanahusu uchapaji wa fomu za kutoa ripoti, kuwa na njia za kuripoti udanganyifu; kujenga minada ya ukaguzi wa bidhaa gatini kwenye bandari; na kuweka njia za mawasiliano mtandaoni. Uchambuzi wa ruwaza unaweza kuonyeshwa kwenye mchoro hapa chini.

Kielelezo 1: Majukumu ya mamlaka ya Ushuru na Mapato na Wajibu wa Mlipa Ushuru

Ushuru na Mapato	Wajibu wa Mlipa Kodi
1. Kutoa habari sahihi kuhusu ulipaji ushuru 2. Kuelimisha walipa kodi 3. Kutoa machapisho kuhusu ulipaji, kutoa ripori ya mapato na kudai pesa kutoka kwa mamlaka ya ushuru 4. Kutoa mbinu rahisi za ulipaji kodi 5. Kuajiri, funza na eneza maafisa katika mamlaka ya kutoza kodi 6. Kujibu maswali ya raia kuhusu ulipaji kodi kwa haraka	1. Kujisajili kama mlipa kodi 2. Kulipa ushuru 3. Kutoa ripoti sahihi ya mapato yako na ushuru unaolipa

Majukumu ya mamlaka ya mapato ni madai ya mlipa ushuru wakati majukumu ya mlipa ushuru ni maombi ya mamlaka hiyo kwa mlipa ushuru. Hapa chini kuna uchambuzi wa ziada wa muundo, wa wafanyabiashara na mamlaka ya manispaa.

Kielelezo 2: Wajibu wa Mamlaka za Manispaa na Wafanyibiashara

Majukumu ya Manispaa (Madai ya Wafanyibiashara)				
Kujenga na kuendeleza ubora wa barabara	Kutoa habari kuhusu riba za ushuru, kodi za nyumba na jinsi ya kuzilipa	Kuwatendea wafanyi biashara kwa heshima na ustahifu	Kuandaa huduma za umma k.m. taa za barabarani, kuondoa maji chafu na kuokota taka	Kudumisha usafi kwa kuweka vioo na mapipa ya taka katika vituo vya biashara
Majukumu ya Wafanyabiashara (Madai ya Mamlaka ya Manispaa)				
Kulipia leseni za biashara husika	Kuzingatia kanuni za usajili, ukaguzi, afya na usalama	Kulipa kodi na ada kwa muda uliowekwa	Kukubaliana na wafanyakazi wa manispaa kufikia maeneo ya biashara kwa ajili ya ukaguzi	Kutupa takataka katika vituo vilivyotengwa

2.3 Hatua ya Tatu: Uchambuzi wa Upungufu wa Uwezo

Uwezo unarejelea kuwa kwa wenye haki kudai haki zao na wanaotekeleza majukumu kufanya kutekeleza majukumu yao. Katika mfano wa kutosajili, kuna haja ya kufichua ni nini kinachozuia walipa ushuru kujisali na vile vile kinachozuia mamlaka ya ushuru kuwatambua na kuwasajili. Matokeo haya yanatumika kubainisha jinsi vikwazo hivi vinaweza kushughulikiwa, hasa kwa kuendeleza ujuzi unaokosekana chini ya masharti matano yafuatayo, ambayo ni:

- **Wajibu -** Kukubalika na kujumuisha jukumu au wajimu.
- **Mamlaka -** Kuwa na uwezo, ruhusa, na nafasi ya kutenda.
- **Rasilimali -** Kuwa na vifaa vya utendaji kama vile, wafanyakazi, ujuzi, maarifa, muda, teknolojia, mitambo, mifumo na sheria.
- **Kufanya maamuzi -** Kuchagua jinsi ya kuendelea.
- **Mawasiliano -** Kupata habari na njia za mijadala.

Haya yameelezewa hapa chini kutumia ulipaji ushuru kama wajibu.

Jedwali 3: Ulipaji Ushuru kama Wajibu

Kipengele cha Uwezo na Ujuzi	Kwa Mamlaka ya Kutoza Ushuru	Kwa Mlipa Kodi
Wajibu	• Kutimiza wajibu wa kusajili walipa kodi zaidi	• Kukubali kwamba kulipa kodi ni wajibu wa raia
Mamlaka	• Kutumia sheria inayohitaji usajili wa walipa kodi	• Kukubali kwamba malipo ya ushuru huanza kwa kusajiliwa
Rasilimali	• Kuanzisha vyanzo vya habari kuhusu walipa kodi watarajiwa kwa mfano, rejista za biashara, mali, kadi za utambulisho, wachangiaji wa hifadhi ya jamii na watumiaji wa simu za mkononi • Kuwa na wafanyikazi, ofisi na mitambo	• Kusoma sheria za ulipaji ushuru na taratibu za ushuru • Kutafuta ushauri kutoka kwa mawakala na maafisa wa ushuru
Kufanya maamuzi	• kuchagua mbinu za kusajili walipa kodi kama; taarifa kwa umma; au usajili kwa wingi mara kwa mara	• Kujifichua kwa mamlaka ya ushuru • Kuhudhuria baraza za kuelimisha walipa kodi
Uwezo wa kufanya mawasiliano	• Kusambaza habari kuhusu jinsi, wapi, na wakati wa kujisajili	• Kutafuta habari sahihi kuhusu vyeti vinavyohitajika kwa usajili

2.4 Hatua ya Nne: Kutambua Vipaumbele vya Kutekeleza

Suluhu bora zilizotambulika kutokana na uchanganuzi wa upungufu wa uwezo zinatathminiwa kwa umuhimu, utekelezaji na dharura. Kisha hupewa kipaumbele na kupangwa ifaavyo kulingana na maudhui. Kwa mfano, mamlaka ya ushuru inaweza kutafiti kuhusu walipa ushuru watarajiwa, kuzindua kampeni ya uhamasishaji, na kuanzisha vituo vya usajili.

2.5 Hatua ya Tano: Muundo wa Programu

Hii inahusu kuweka hatua katika mpango madhubuti kuhusu mikakati kama vile: uhamasishaji; habari na mawasiliano; mafunzo; na mifumo na miundombinu. Kisha programu inatekelezwa na kutathminiwa kwa kuzingatia matatizo yaliyoainishwa kutokana na uchambuzi wa sababu yazo.

3.0 Mitindo ya Haki za Binadamu katika Ulipaji Ushuru kwa Miktadha ya Dharura

Nchi mara nyingi hukumbwa na hali isiyo ya kawaida kama vile majanga yanayosababishwa na binadamu, majanga ya kimaumbile, milipuko wa magonjwa na vita. Hali hii hupunguza uwezo wa wananchi wa kuendelea na biashara na kulipa ushuru pamoja na uwezo wa serikali wa kukusanya ushuru na kutoa huduma. Kama ilivyobainishwa katika miradi ya maendeleo (2019),

> ***Hasara inayopatika kutoka kwa majanga inaweza kuwa ya kiuchumi, kimazingira na kijamii. Hasara za kibinadamu na kiuchumi kutokana na majanga hupunguza tija ya kiuchumi ya jumla na hutatiza ubora wa maisha ya wananchi huku ikiwazamisha zaidi kwenye umaskini.***

Ni muhimu kubainisha kuwa majanga hayatupilii mbali haki za binadamu. Kwa kweli, yanaimarisha umuhimu wa kuheshimu, kulinda na kuzitimiza. Kutokana na utafiti wa mikakati ya kupunguza hasara ya majanga uliofanywa katika kaunti nne za kenya, utafiti ulizindua kuwa matumizi yaliyopewa kipaumbele ya maji, elimu na afya ni vipengele vya Haki za Kiuchumi, Kijamii na kitamaduni, *"unaimarisha uwezo wa wakaazi kustahimili misukosuko"* kwa kuboresha mbinu za kukabiliana.

Hata hivyo, kiwango ambacho haki za binadamu zinazingatiwa hubadilika kulingana na mafundisho ya kudharauliwa - kuwa serikali inaweza kutupilia mbali au kupunguza baadhi ya haki ili kulinda maisha ya binadamu, ihakikishe ulinzi na usalama na kudumisha sheria na utaratibu kwa kipindi maalum kulingana na sheria zilizopo. Lakini haki zingine haziwezi kujadiliwa, ya msingi zaidi ikiwa haki ya kuishi.

Mfano mwafaka wa dharura ambayo ilichangia kupunguzwa kwa haki ni janga sugu la virusi vya korona (COVID-19) vilivyochipukia Uchina Disemba 2019. Ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa huu, serikali ziliweka mikakati ya kupunguza usafiri na utangamano wa watu. Kwa kufanya hivyo, zilipunguza haki za kutembea na kutangamana. Mikakati kama hii ilikuwa kwenye mojawapo ya majukumu ya kulinda maisha ya wananchi. Kukosa kuchukua mikakati hii itakuwa ni ukwepaji wa majukumu. Muktadha huu unachangia kuchipuka kwa maswala mawili mengine: ulipaji ushuru na utoaji wa huduma.

Janga hili halikutupilia mbali jukumu la kulipa ushuru. Hata hivyo, serikali zilipaswa kutambua kuwa wananchi wengi walipoteza vyanzo vya mapato na uwezo wa kulipa ushuru. Kwa kweli, wengi walihitaji msaada ili kukidhi mahitaji yao ya kimsingi. Kwa kuwajibika, serikali kadhaa ziliweka mikakati ya dharura ya ulipaji ushuru ili kuwasaidia wananchi na kudumisha maisha.

Ulimwenguni, mikakati hii ilijumuisha: fedha za kuinua uchumi ili kusaidia Biashara Ndogondogo na zile za Wastani (SME); kuhairisha wajibu wa ulipaji ushuru na kodi mbalimbali; ruzuku kwa wafanyakazi na misaada ya mishahara au ya mapato kwa wafanyikazi; na kutoa fedha za msaada kwa familia OECD (2020) inabainisha, kwa mfano, kuwa Marekani ilitoa *"uhamisho wa fedha kwa familia zenye mapato ya chini na ya kati".* Mataifa ya Afrika Mashariki yalitekeleza mikakati mbali mbali ili kupambana na athari za ugonjwa huu.

Nchini Kenya, serikali ilipunguza kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka 14% hadi 16%; ushuru wa shirika kutoka asilimia 25 hadi 30; kodi ya mauzo katika biashara ndogo na za wastani kutoka asilimia 3 hadi 1; na kiwango cha juu zaidi cha mapato ya kibinafsi kwa asilimia 5. Ilitoa agizo la kupunguzwa kodi kwa asilimia 100 kwa mishahara ya kila mwezi kwa wenye hupokea shilingi za Kenya 24,000 (dola 240) na kuelekeza Mamlaka ya Mapato Kenya (KRA) kulipa madai yaliyodhibitishwa ya kodi ya ongezeko la thamani kwa biashara kwa muda wa wiki tatu kutoka Machi 25, 2020 ili kudumisha mzunguko wa pesa.

Iliendelea kwa kuimarisha miradi ya mikopo kwa biashara ndogondogo pamoja na za wastani na kuomba kampuni kwenye sekta ya kibinafsi kuweka mikakati kukabiliana na hali hii. Katika suala hili, kampuni kubwa ya kimawasiliano ya *Safaricom* ilitupilia mbali ushuru katika uhamisho wa fedha kwa njia ya simu za rununu kwa kiwango cha shilingi za Kenya 1,000 (dola 10) kurudi chini. Serikali pia ilianzisha mfumo wa kuzipa familia zisizojiweza shilingi 1000 (dola 10) kila wiki.

Zaidi ya hayo, kudhibiti janga hili kulihitaji kunawa mikono mara kwa mara na kutumia viyeyuzi. Hili halingeweza kufanyika bila kufikiwa kuwa na maji safi na yenye uhakika. Katika nadharia ya haki za binadamu, kupata na mji huashiria sio tu kupatikana, bali utoshelevu na ubora. Kutambua kuwa idadi kubwa ya watu mijini, hasa wale walio kwenye makazi yasiyo rasmi, hawangeweza kupokea haki hii ikiwa wangehitajika kulipa, serikali iliamrisha watoa huduma za maji kuweka makubaliano ya kutofunga maji katika msimu wa janga. Vinginevyo, haingekuwa na maana kuwashurutisha watu kunawa mikono bila maji. Isitoshe, serikali za kaunti ziliunda vifaa na kutenga maeneo ya umma ya kunawia mikono, na kusafirisha maji bila malipo kupelekea wananchi wasiokuwa na maji. Kwa kufanya hivi, jambo hili lilipoteza ushuru ambao ungekusanywa katika hali ya kawaida na kukidhi wajibu wa kutimiza haki ya kupata maji, na kwa upana chakula, afya na uhai.

Rwanda ilijibu kwa: kuunda Mpango wa Kufufua Uchumi uliogharimu asilimia 3.3 ya pato la taifa; mpango wa usambazaji wa chakula wa nyumba hadi nyumba mara mbili kwa wiki; usambazaji wa fedha kwa wafanyakazi wa kibarua; ruzuku kwa bidhaa za kilimo; mikakati ya ufikiaji wa afya na elimu kwa familia maskini; mikopo yenye ruzuku kutoka kwenye taasisi za fedha; kukubaliana jinsi ya kukusanya madeni yaushuru; kuongezwa kwa tarehe ya mwisho ya kutoa ripoti ya mapato na kiwango cha ushuru; kuongeza kasi ya urejeshaji wa VAT kwa biashara; na kuondolewa kwa ushuru kwa walimu wa shule za kibinafsi na wafanyakazi katika sekta ya utalii na hoteli wanaopata kiwango fulani cha mapato. Pia ilitoa muda wa siku 30 wa kukomaa kwa malipo ya mpango wa bima ya Afya ya Umma ili kuhakikisha huduma za afya zinafikiwa.

Serikali ya Tanzania iliharakisha malipo ya malimbikizo ya matumizi yaliyothibitishwa kwa wafanyabiashara wadogowadogo na wa kati ya hadi kufikia dola za Marekani milioni 376 mwezi Machi 2020, na kupanua mifumo ya hifadhi ya jamii kwa dola za Marekani milioni 32.1 ili kuwawezesha wale waliokosa ajira kutokana na janga hili kuendeleza shughuli zao bila matatizo. Pia iliondoa ushuru wa VAT na ushuru wa forodha kwa vifaa na bidhaa za hospitalini.

Uganda iliongeza bajeti mbili za ziada kwa karibu dola milioni 370 ili kusaidia sekta muhimu na makundi yasiyojiweza. Hili lilitekelezwa kwa kufadhili bidhaa za kilimo, ufadhili zaidi wa biashara ndogondogo na za wastani ili kuongeza mapato ya familia. Pia, ilitupilia mbali malipo ya kodi ya wafanyakazi, iliondoa

riba kwa kodi iliyokuwa haijalipwa, iliharakisha urejeshaji wa pesa zilizotozwa kwenye kodi ya ongezeko la thamani, iliongeza ufadhili kwa mipango ya afya, chakula kwa watu wasiojiweza na ulinzi wa kijamii.

Mikakati ya Burundi ilijumuisha kuondolewa kwa ushuru kwa mahoteli na viwanda visivyo na uwezo wa kulipa pamoja na ruzuku kwa mishahara ya wafanyikazi waliopoteza ajira.

4.0 Hitimisho

Wadau wa haki ya kodi kama vile Mtandao wa Ushuru na Utawala wa Afrika Mashariki, wanachama wake, asasi za kiraia, vyombo vya habari, taasisi za elimu, na wanaharakati wanaweza kuchangia ufahamu wa suala la ulipaji ushuru kama suala la haki za binadamu na kuwezesha mamlaka ya ushuru kutekeleza wajibu wake kulingana na viwango na kanuni za haki za binadamu. Hii inafaa kujumuisha kubadilisha lugha ya usimamizi wa kodi kutoka kwa mfumo wa "masharti na madhara" hadi kwa ule wa kufahamu majukumu. Katika suala hili, wadau wa haki ya kodi hawapaswi tu kuona wajibu wao kama kuanzia kwa mtu mzima bali kwa mtoto ambaye atakua na kuwa mlipa ushuru.

Kuelimisha mtoto aelewe ulipaji ushuru ni nini, umuhimu wake, wajibu wa kimaadili wake na pia haki zinazojitokeza kwa kutimiza jukumu hili inaweza kubadilisha uhusiano kati ya wananchi na serikali kutoka ule wa uadui na kuwa wa kushirikiana na wote kufanya kazi pamoja kwa ubora wa jamii. Kwa muktadha huu, mamlaka ya kodi haitajiona kuwa wawakilishi wa serikali tawala bali kama wasaidizi wa wananchi kukuza taifa lao. Kama mbinu ya kukuza utamaduni huu, mamlaka ya kodi haitaripoti tu kufikia kwa lengo la ushuru uliokusudiwa bali kueleza mbinu walizotumia na jinsi wanavyokuza haki za binadamu.

Hii itahitaji kuripoti juu ya idadi na asili ya migogoro iliyopokelewa na kutatuliwa, idadi ya walipa kodi walioridhika na utatuzi wa migogoro, uboreshaji wa viwango vya ulipaji ushuru, mabadiliko ya tabia na mitazamo ya wafanyakazi wa ushuru kwa walipa ushuru (na kinyume chake) na yaliyomo, lugha, na picha za nyenzo za mawasiliano ya habari kwa umma. Hii inaweza hata kujumuisha uanzishwaji wa ofisi za haki za binadamu na mamlaka ya ushuru. Kwa muda mrefu, kuanzishwa kwa mtazamo wa haki za binadamu kwa kodi kungefikia kilele katika sheria za kitaifa na kimataifa kuhusu haki za binadamu na ushuru.

5.0 Mapendekezo

Kama hatua ya kwanza, EATGN itafanya kazi kujenga uwezo wake wa ndani kuhusu Mbinu inayozingatia Haki za Binadamu miongoni mwa wanachama wake na kufuatilia utendakazi wa mbinu zake za kimkakati kupitia shughuli madhubuti zinazokuza mbinu hiyo. Kwa mfano, itafanya mambo yafuatayo chini ya mbinu tatu katika mpango wake wa kimkakati wa 2019 - 2023.

5.1 Utafiti

1. Kufanya utafiti kuhusu ni kwa kiasi gani mamlaka ya ushuru katika eneo la Afrika Mashariki inaelewa, kutumia, na kutekeleza mbinu zinazozingatia haki za binadamu katika usimamizi wa ushuru.
2. Kushirikiana na mamlaka za ushuru katika eleo la Afrika Mashariki kubainisha na kufanya tafiti mahususi ili kuboresha matumizi ya mbinu zinazozingatia haki za binadamu katika usimamizi wa ushuru.
3. Kufanya tafiti juu ya haki ya ushuru kwa mtazamo wa kijinsia.
4. Kufanya utafiti wa mbinu za kuimarisha ari ya kodi kupitia mbinu zinazozingatia haki za binadamu.

5.2 Mawasiliano na Usambazaji

1. Kuunda hazina ya mazungumzo juu ya haki za binadamu na ushuru.
2. Kusambaza utafiti kuhusu ushuru na haki za binadamu.
3. Kufanya mijadala ya kisera kuhusu ushuru na haki za binadamu kuelekea kwa sera na sheria mpya.

5.3 Mafunzo na Kujenga Uwezo

1. Kutoa mafunzo kwa mashirika wanachama juu ya Mbinu inayozingatia Haki za Binadamu na matumizi yake kwa haki ya ushuru.
2. Kutoa mafunzo kwa umma kuhusu ushuru kama suala la haki za binadamu.
3. Kushirikiana na taasisi za elimu ili kuunda kizazi cha baadaye cha walipa ushuru kupitia elimu ya haki za binadamu.

6.0 Marejeleo

Amnesty International Netherlands (AIN), *Haki Zetu Main Book, Part 1*. Amsterdam: AIN, 2010, https://www.amnesty.nl/content/uploads/2017/01/the_right_to_work_and_livelihood_light.pdf?x76291.

Bagenda E, *A human rights approach to taxation: some brief comments In Africa Tax Spotlight*. Tax Justice Network, 2011, https://www.taxjustice.net/cms/upload/pdf/Africa_Tax_Spotlight_6th_edition.pdf.

Development Initiatives, *Tracking Subnational Government Investments in Disaster Risk Reduction in Kenya*. Nairobi: Development Initiatives, https://www.preventionweb.net/publication/tracking-subnational-government-investments-disaster-risk-reduction-kenya

East Africa Tax and Governance Network (EATGN), T*axing Rights Policies are Human Rights Policies*. Nairobi: EATGN 2017, https://www.eataxgovernance.net/wp-content/uploads/2020/03/EATGN-Tax-and-Human-Rights-Report.pdf

East African tax and Governance Network (EATGN). *Priorities for the Region: Strategic Plan of the East Africa Tax and Governance Network 2019-2023*. Nairobi: EATGN 2019.
https://www.eataxgovernance.net/wp-content/uploads/2020/03/R-Priorities-For-The-Region-Strategic-Plan-of-th-East-Africa-Tax-and-Governance-Network-compressed-1.pdf

Feinberg, J, *Doing and Deserving: Essays in the Theory of Responsibility. Princeton: Princeton University Press,* 1970.

Hohfeld WN, *Fundamental Legal Conceptions as Applied in Judicial Reasoning and Other Legal Essays*. Yale University Press, New Haven – Connecticut 1966 (Reprint from *Yale Law Journal*), (1913, 1917).

Jonsson U, *Human Rights Approach to Development Programming*. Nairobi: UNICEF ESARO, 2003. https://hrlibrary.umn.edu/research/Egypt/HRBDP_Urban_Jonsson_April_2003.pdf

Kenya Revenue Authority (KRA), Service Charter. Nairobi: KRA, 2019.
https://kra.go.ke/images/publications/SERVICE-CHARTER-New.pdf

Organisation for Economic Co-operation and Development (OECD), *Tax and Fiscal Policy in Response to the Coronavirus Crisis: Strengthening Confidence and Resilience*. https://www.oecd.org/en/publications/tax-and-fiscal-policy-in-response-to-the-coronavirus-crisis-strengthening-confidence-and-resilience_60f640a8-en.html. Accessed on June 30, 2020.

Rwanda Revenue Authority (RRA). Service Charter.
https://www.rra.gov.rw/fileadmin/user_upload/rra_service_charter_2.pdf

Tanzania Revenue Authority (TRA), Taxpayers Service Charter 2017 (8th Edition). Dar es salaam: TRA, 2017. https://tata.or.tz/wp-content/uploads/2024/06/TAXPAYER-SERVICE-CHARTER.pdf

Uganda Revenue Authority (URA), The Client Service Charter. Kampala: URA, 2020.
https://www.scribd.com/document/543871073/10118-URA-Client-Service-Charter-1

United Nations Office for Disaster Risk Reduction (UNDRR), *Disaster Risk Reduction Investment in Africa – Evidence from 16 Risk-sensitive Budget Reviews*. Geneva: UNDRR, 2020.
https://www.undrr.org/publication/disaster-risk-reduction-investment-africa-evidence-16-risk-sensitive-budget-reviews

EATGN inashukuru kwa msaada wa Open Society Foundation (OSF) na NORAD chini ya kampeni ya Scaling Up Tax Justice (SCUT) iliosimamiwa na Tax Justice Network Africa (TJNA)

TAX JUSTICE NETWORK AFRICA

Norad

STOP the BLEEDING

ISBN 978-9914-9995-6-3